

# Taasisi za umma zasisitizwa kujiunga mfumo wa kidijitali

## Na MWANDISHI WETU

MENEJA Mawasiliano Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), Subira Kaswaga, ametoa wito kwa taasisi za umma kujiunga na mfumo wa ubadilishanaji taarifa serikalini (GovESB), ziwasiliane na kubadilishana taarifa kidijitali kupitia mfumo huo.

Kaswaga alitoa wito huo Jana mkoani Mbeya alipozungumza kuhusu huduma zinazotolewa na e-GA katika Maonesho ya Wiki ya Wakulima ambayo mwaka huu yanafanya kitaifa jijini humo.

Alisema mfumo wa GovESB ni shirikishi na unaziwezesha taasisi za umma kuunganisha mifumo yao ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), kupitia mfumo huo kuzungumza na kubadilishana taarifa kidijitali.

"Falda za mfumo huo ni kuongeza ufanisi wa utendaji kazi katika taasisi za umma, kuokoa muda, gharama za uendeshaji wa taasisi na kurahisisha utoaji huduma kwa wananchi kwa wakati," alieleza.

Allongeza: "Mfumo wa GovESB ni jitihada

za mamlaka kuhakikisha mifumo ya tehma katika taasisi za umma inazungumza na kubadilishana taarifa kupunguza urudufu wa mifumo serikalini, hivi sasa taasisi za umma zimeunganisha mifumo yake na GovESB, lakini zipo taasisi ambazo bado hazijaunganisha, hivyo nitoe wito zijiunge," alisema.

Alibalnisha e-GA imedhamiria kuhakikisha utekelezaji wa jitihada za Serikali Mtandao katika taasisi za umma unaimarika na kuboresha utoaji huduma kwa wananchi.

"Mamlaka imedhamiria kuhakikisha mwananchi anapata huduma zote za serikali kidijitali mahali alipo, kufikia malengo hayo, tunashirikiana na taasisi za umma kutengeneza mifumo ya kisekta itakayosaidia utendaji kazi katika taasisi hizo," alisitisiza.

Naye, Ofisa TEHAMA wa e-GA, Caesar Mwambani alisema mamlaka ya serikali mtandao kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, imetengeneza mfumo wa



**Mamlaka imedhamiria kuhakikisha mwananchi anapata huduma zote za serikali kidijitali mahali alipo, kufikia malengo hayo, tunashirikiana na taasisi za umma kutengeneza mifumo ya kisekta itakayosaidia utendaji kazi katika taasisi hizo.**

Meneja Mawasiliano Mamlaka ya Serikali Mtandao, Subira Kaswaga.

e-Mrejesho unaowawezesha wananchi kuwasiliana na serikali kidijitali.

Alisema mfumo huo unawawezesha wananchi kuwasilisha maoni, changamoto,

pongezi au malalamiko kwenda katika taasisi yoyote ya umma na kufuatilia utekelezaji wake kupitia mfumo huo.

"Mfumo huu unamrahisishla mwananchi kuwasiliana na serikali kidijitali na hivyo kumpunguzia gharama za kusafiri kwenda katika taasisi husika kuwasilisha kero yake na badala yake anaweza kuwasiliana na taasisi hiyo kupitia mfumo wa e-Mrejesho popote alipo," alisema.

Allongeza mfumo wa e-Mrejesho unapatikana kupitia tovuti ya [www.emrejesho.go.tz](http://www.emrejesho.go.tz), simu janja kwa kupakua aplikesheni yake au kwa namba ya msimbo kwa kupiga \*152\*00# na kuchagua namba tisa, kisha namba mbili na kuwasilisha hoja kwa taasisi husika.

Mamlaka ya serikali mtandao imeanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Serikali Mtandao Na. 10 ya 2019 ikiwa na jukumu la kuratibu na kusimamia utekelezajia wa sera, sheria, kanuni, viwango na mlongozo ya serikali mtandao katika taasisi za umma.